**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1155


# Mofosemantiki na dhima ya Majina ya Ng'ombe kwa Kigezo cha Rangi: Mifano kutoka Jamiilugha ya Ginantuzu

**Njana Masanja**
*Mwalimu Nyerere Memorial Academy, Tanzania*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-02-05
Kurekebishwa: 2025-07-14
Kukubaliwa: 2025-07-15
Kuchapishwa: 2025-07-16

**Maneno Muhimu**
Dhima
Majina
Mofosemantiki
Ng'ombe

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Masanja, N. (2025). Mofosemantiki na dhima ya Majina ya Ng'ombe kwa Kigezo cha Rangi: Mifano kutoka Jamiilugha ya Ginantuzu. *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 3*(2), 30-44.

Copyright © 2025

**Ikisiri**
Makala hii inahusu uchunguzi wa mofolojia na semantiki katika majina ya ng'ombe kwa kigezo cha rangi hususani katika jamiilugha ya Ginantuzu. Lengo kuu la makala hii ni kubainisha maumbo yaliyomo katika majina ya ng'ombe, maana na dhima za majina ya ng'ombe. Utafiti huu ulifanywa katika mkoa wa Simiyu, wilaya ya Bariadi vijijini. Jumla ya vijiji viwili vilipitiwa na mtafiti. Vijiji hivyo ni Ihusi na Nkindwabiye. Sampuli ya watoataarifa sita (6) iliteuliwa na mtafiti kwa ajili ya mahojiano ili kukidhi lengo la makala hii. Kwa kutumia usampulishaji lengwa wastani wa watoataarifa (3) kwa kila kijiji walipatikana. Watoataarifa waliteuliwa kwa kuzigatia kigezo cha usampulishaji lengwa. Data za uwandani zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano, ushuhudiaji na mapitio ya nyaraka za maktabani na mitandaoni. Ili kufanikisha kazi hii, makala ilitumia nadharia ya Semeotiki iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure. Aidha, Mkabala wa kitaamuli ndio umetumiwa kubainisha maumbo, maana na dhima za majina ya ng'ombe. Matokeo yameonesha kuwa majina ya ng'ombe dume yameundwa kwa mashina ya ng'ombe jike kwa kuongezewa mofu tangulizi inayobeba maana ya dume. Jumla ya alomofu tatu zinazobanisha jinsia ya kiume zilipatikana. Alomofu hizo ni **gí-, gid-** na **gida-.** Mwisho makala hii inapendekeza uchunguzi zaidi wa kiisimu kuhusu utoaji wa majina ya mifugo kuendelea kufanyika ili kuimarisha mawasiliano katika jamii mbalimbali za wafugaji na kuyahifadhi majina hayo kwa ajili ya vizazi vijavyo.

## Utangulizi

Kila kiumbe na hali hupewa jina na binadamu ili kusaidia utambuzi wa haraka wa kile kinachorejelewa Masanja (2025). Majina ni utambulisho ambao ni uwakilishi wa sauti kwa herufi katika maandishi (tahajia) ya majina ya watu, vitu, wanyama, mimea na hata pahala. Massamba (2004) anasema kuwa; *Jina ni aina ya neno linalotaja au kubainisha viumbe hai, vitu visivyo uhai, mahali, hisia, maarifa au tukio katika tungo*. Jina ni kipengele muhimu cha maisha, utambulisho na utamaduni wa binadamu katika jamii mbalimbali za kiafrika.

Ginantuzu ni lugha inayozungumzwa katika mkoa wa Simiyu uliopo Kanda ya ziwa Victoria nchini Tanzania. Mzungumzaji wa lugha huitwa Munantuzu (wingi wake ikiwa ni Bhanantuzu). Ginantuzu ni miongoni mwa lahaja inayopatikana katika lugha ya Kisukuma. Lahaja hii kwa jina jingine inajulikana kama *Kimnakiiya* iliyopewa msimbo wa F.21C (Batibo, 1976). Kiasili lahaja ya Ginantuzu inazungumzwa Mashariki mwa eneo la usukumani katika wilaya ya Bariadi, Itilima na

baadhi ya maeneo ya wilaya za Meatu, Maswa na Busega. Lahaja zingine katika lugha ya Kisukuma ni Gimnanasa (Kimnang'weli), Ginang'wagala, na Ginadakama (Mabondo, 2012)

Hamasa ya kuchunguza utoaji wa majina ya ng'ombe katika Ginantuzu imesababishwa na uchunguzi wa Simon, C. (2024) aliyechunguza maana na asili ya majina ya ng'ombe katika kabila la Wasukuma kwa ujumla. Utafiti wake ulijikita zaida kuchunguza maana na asili ya majina ya ng'ombe tu bila kuangalia vipengele vingine. Makala hii inajikita kuangalia mofolojia, semantiki na dhima ya majina ya ng'ombe dume na jike kwa kigezo cha rangi katika lahaja ya Ginantuzu.

Kimsingi suala la dhana ya majina ya mifugo ni mada ambayo imewavutia wanaisimu wengi duniani kote. Wataalamu kama Olson (1964) alichunguza majina ya ng'ombe dume katika Gịrịmi. Ohta (1987) alichambua utoaji wa majina kwa wanyama katika jamii ya Turkana iliyopo Kaskazini Mashariki mwa Kenya na Imai (1982a) alibainisha majina ya kondoo, mbuzi, ngamia na ng'ombe kwa kutumia kigezo cha hali ya mnyama husika katika jamii ya Gabra. Imai (1982b) alitafiti kuhusu utoaji wa majina ya mbuzi katika jamii ya Gabra huku Mustefa na wenzake (2023) walichunguza tofauti zinazopatikana katika ng'ombe wa Harar na Ogaden Mashariki mwa Ethiopia. Watafiti wengine waliojihusisha na kuchunguza majina ya mifugo ni Magoro na wenzake, (2022) waliochunguza utofauti wa maumbile na uhifadhi katika aina za mbuzi wa asili wa Afrika kusini. Peacock (2005) alibainisha umuhimu wa ufugani wa mbuzi kama nyenzo ya kupunguza umasikini Afrika wakati Monau na wenzake (2020) walichunguza uendelevu wa matumizi ya mbuzi Afrika kusini kwa kutaja wachache.

Ohta (1987) katika utafiti wake alichunguza utambuzi na utoaji wa majina kwa wanyama katika jamii ya Turkana iliyopo Kaskazini Mashariki mwa Kenya. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa, kigezo kikubwa kabisa cha kutoa majina kwa wanyama ni umri na ujinsi. Vigezo vingine ni rangi ya ngozi, umbo la pembe na umbo la sikio. Kuhusu umri na ujinsi, Ohta (1987) anasema kwamba kuna hatua kubwa tatu za ukuaji wa wanyama ambazo huambatana na utoaji wa majina. Katika hatua ya kwanza, ng'ombe dume na jike wanakuwa na majina yanayofanana hata kama jinsi zao zinatambulika. Katika kutofautisha majina kijinsia anasema, ***lokile*** hutumika kwa dume na ***naberu*** kwa jike. Majina haya huwekwa mwishoni mwa jina ili kufafanua mnyama anayerejelewa ni wa jinsia ipi. Jinsia hutofautishwa kwa viambishi awali ***lo-*** (dume), ***na-*** (jike).

Kuhusu kigezo cha rangi, Ohta (1987) anasema kuwa kuna rangi mbalimbali za ngozi. Rangi hizo ni -aakwan (nyeupe), -kiryoon (nyeusi), -aaryangan (nyekundu), nyang (njano au machungwa), -ngori (kijivu au kahawia), -kipurat au -bok (nyekundu na zambarau mpauko). Rangi hizo ndizo zinazotumiwa katika kutoa majina. Hata hivyo, baadhi ya ng'ombe huwa na rangi zaidi ya moja; kwa hiyo, ng'ombe hao hupewa majina kwendana na rangi zilizopo kwenye ngozi. Mathalani, -meri hutaja ng'ombe mweupe mwenye vidoa vyeusi (-kiryoon), ng'ombe mwenye rangi za bluu na kijani ataitwa (-pus), na zambarau (-mugi) na -kori hutaja ng'ombe wa rangi nyekundu (-aryangan), njano (-nyang), kijivu (-ngori) na nyekundu zambarau mpauko (kipurat au -bok).

Ingawa utafiti wetu hauhusiani na kuchunguza majina ya ng'ombe kwa kigezo cha umri kakini matokeo ya utafiti huu yalitusaidia kuibua ari ya kwenda uwandani ili kuchunguza mofosemantiki na dhima katika majina ya ng'ombe kwa kigezo cha rangi kutoka jamii lugha ya Ginantuzu. Mchango wa utafiti huu unaunga mkono hoja iliyopo katika kuchunguza mofosemantiki na dhima ya majina ya ng'ombe kwa kigezo cha rangi kutoka jamii lugha ya Ginantuzu.

Imai (1982b) katika utafiti wake alichunguza utoaji wa majina ya mbuzi katika jamii ya Gabra. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa jamii ya Gabra hutoa majina ya mbuzi kwa kuzingatia jina la kikeni (majina ya kutoka upande wa kike), yaani, mbuzi jike huitwa kwa jina la ukoo wa upande wa mama (mfumo jike). Kwa hiyo, kila mbuzi huitwa kwa jina la mama yake. Jina la

kwanza la mbuzi ni la ukoo (kikeni) na jina la pili linatokana na mwonekano wa mbuzi kama rangi na pembe. Rangi zinazotumika katika Gabra ni kama vile adi (nyeupe), dimtu (kahawia), ble (kijivu), na grati (nyeusi). Kwa hiyo, mbuzi akiitwa adio moyeti, adio linakuwa la ukoo (ukoo mweupe) na moyeti ni hali ya kutokuwa na pembe (jina la mwonekano.

Matokeo ya utafiti huu umetusaidia kufahamu kuwa mbuzi kama mfano wa mifugo wanaitwa kwa namna mbalimbali kama vigezo vya ukoo na mwonekano wa mnyama kama rangi na pembe. Utafiti huu una tija kubwa katika kuandika makala yetu kwa sababu unaelekeza na kubainisha majina ya wanyama kwa kuangalia kigezo cha rangi ambacho tulikitumia katika utafiti wetu.

Mustefa na wenzake (2023) walichunguza tofauti zinazopatikana katika ng'ombe wa Harar na Ogaden Mashariki mwa Ethiopia. Matokeo ya utafiti wake yalionesha kuwa ng'ombe wa Harar walikuwa na pembe zilizoelekea mbele, zilizo na nafasi pana na urefu waka huku ngombe wa Ogaden walikuwa na pembe fupi zilizonyooka zilizo na nafasi ndogo. Utafiti pia ulionesha kuwa ng'ombe wa Harar walikuwa na mchanganyiko wa rangi nyingi kama nyekundu, nyeupe na nyeusi wakati ng'ombe wa Ogaden walikuwa na rangi ya kijivu. Matokeo ya utafiti huu yalitusaidia kwa kiasi fulani hasa kipengele cha rangi za ng'ombe kitu ambacho ni miongoni mwa vigezo vinavyotumika kuhusu makala hii.

**Nadharia ya Semiotiki**

Semeotiki ni nadharia inayohusiana na mfumo wa ishara. Nadharia hii inajumuisha uchunguzi, uelewa na utabiri wa maana za ishara na namna zinavyopatikana katika vitu halisi. Kwa ujumla semeotiki ni nadharia inayojishughulisha na utoaji wa fasili za maana zinazolenga ishara mbalimbali katika lugha. Nadharia hii ya kiisimu imeasisiwa na mwanazuoni wa kiisimu Ferdinand de Saussure mwaka 1857. Mwanzilishi huyu ni miongoni mwa wanafalsafa wa Kipragmatiki mzaliwa wa Uswizi aliyeishi na kukulia Marekani. Kwa mujibu wa Ferdnand de Saussure (1976) anasema kuwa msingi mkubwa wa nadharia hii inahusu ni kufafanua lugha kama mfumo wa ishara, ambazo huungana na kuunda mkufu wa ishara hizo katika lugha. Hivyo, kila ishara huwa na sehemu mbili, yaani kiashiria (sauti au wasilisho la kimaandishi) na kiashiriwa (maana ya kiashiria). Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kiashiria ni neno lenyewe, na kiashiriwa ni maana inayopatikana kutokana na kiashiria. Kwa mfano neno '**mbuzi**' ni kiashiria na '**mnyama mbuzi'** au **'kifaa cha kukunia nazi'** ndio kiashiriwa chenyewe. Vile vile, De Saussure anaelezea kuwa kiashiria ni picha au sauti, wakati ambapo kiashiriwa ni dhana au maana iliyokusudiwa. Brown (1995) anasisitiza kuwa ishara hupata maana kutokana na matumizi yake. Hivyo watu wa jamii moja, wenye kuzungumza lugha moja na kushiriki utamaduni ulio sawa, huwa na makubaliano kuhusu ishara fulani na maana zake. Ishara hizo hujumuisha picha, rangi, maumbo mbalimbali na hata herufi zinazounda maneno. Sambamba na hayo Griffen (1997) katika kuelezea maana ya maana, aliitumia nadharia hii na kusema kuwa 'ishara ni kama kitu tunachokumbana nacho moja kwa moja na huweza kuashiria kitu kingine tofauti'. Anasisitiza kwamba, majina au maneno huchukuliwa kuwa ni ishara, kwa sababu hupewa maana na watu. Wamitilia na Griffen (wameshatajwa) wanaungama pamoja kwa kusema kuwa, ishara hutumiwa kueleza kitu fulani. Wakiendelea kufafanua zaidi wanaeleza kuwa, ishara huwakilisha kitu kingine katika uhusiano uliopo kati ya vitu hivyo viwili au ni uwezo wa kuibua fikra fulani katika akili ya msomaji. Kwa minajili hiyo, nadharia ya Semiotiki inazungumzia ishara ambazo zinaeleweka na mjuzi wa lugha husika. Nadharia hii ni faafu katika utafiti huu, kwani imetusaidia katika kulifikia lengo letu, kwa vile imetuwezesha kubaini na kuchambua maumbo na maana katika majina ya ng'ombe katika jamiilugha ya Ginantuzu.

**Mbinu za Utafiti**
Makala hii ni matokeo ya utafiti wa kitaamuli kwa kiasi kikubwa na kitakwimu kidogo uliofanyikia maktabani na uwandani. Kwa mujibu wa Walliman (2011), utafiti wa kitaamuli unajikita zaidi na uwasilishaji na uchambuzi wa data kwa kutoa ufafanuzi wake kimaelezo. Mkabala huu umekuwa faafu katika makala hii kwa kuwa tumetumia maelezo ya kiufafanuzi katika kubainisha *mofu*, *maana* na *dhima* katika majina ya ng'ombe katika jamii ya Ginantuzu. Utafiti wa maktabani umetuongoza kupata kazi zinazohusiana na mada ambayo tumeshughulikia. Tumesoma vitabu, makala na kazi mbalimbali zinazotoa maelezo kuhusu mada husika. Data za makala hii zilikusanywa katika mkoa wa Simiyu katika wilaya ya Bariadi vijijini. Jumla ya kata mbili zilifanyiwa uchunguzi. Kata hizo ni Ihusi na Nkindwabiye. Jumla ya vijiji viwili vilipitiwa na mtafiti ambavyo ni Ihusi na Nkindwabiye. Sampuli ya watoataarifa sita (6) iliteuliwa na mtafiti kwa ajili ya mahojiano ili kukidhi lengo la makala. Wastani wa watu watatu (3) kwa kila kijiji walipatikana. Ili kupata sampuli hii, watoataarifa hao walisampulishwa kwa usampulishaji lengwa. Sampuli imechaguliwa kwa uhuru wa mtafiti ili kupata data iliyosaidia kufikia lengo la makala. Data za uwandani, zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano na ushuhudiaji. Mtafiti, katika nyakati tofautitofauti, alifanya mahojiano mbalimbali kuhusu majina ya ng'ombe na kukusanya taarifa kutoka kwa watoataarifa. Uwasilishwaji ulifanywa kwa njia ya maelezo kwa kiasi kikubwa na majedwali kwa kiasi kidogo.

**Dhima ya ng'ombe katika jamii**
Ng'ombe ni mnyama wa jamii ya nyati anayefugwa kwa ajili ya kupata nyama, maziwa, ngozi na kitendea kazi. Katika jamiilugha ya Ginantuzu mnyama huyu ni kitu cha thamani sana kuliko mali nyingine waliyonayo wanajamii. Ukiwa umenunua ng'ombe, mbuzi au kondoo kwa nguvu zako una ruhusu ya kutoka kuikaribisha au kuikemea mvua pale unaposikia ngurumo. Ila kama haujanunua wanyama hawa unatakiwa kunyamaza kimya wakati ngurumo za radi zinaposikika wakati wa mvua.

Kipimo cha utajiri katika jamiilugha ya Ginantuzu ni idadi ya ng'ombe anaomiliki mwanajamii na si kitu kingine. Ng'ombe dume hutumika kulima kwa kutumia plau na kukokota mikokoteni iliyobeba mazao, mizigo na vifaa vya ujenzi. Ng'ombe jike hukamuliwa, ambapo huwapatia wanajamii maziwa, jibini, siagi na samli.

Ng'ombe pia hutolewa kama mahari, kununua mashamba, kulipa fidia na wakati mwingine kuuzwa kwa ajili ya kujipatia fedha kwa matumizi mengine. Kwa mtu ambaye hana ng'ombe na anataka kuoa itabidi atoe pesa inayolingana na bei ya ng'ombe ya wakati huo. Wanajamii hufurahia kusikika wakisema kuwa "Binti fulani ameolewa kwa thamani ya ng'ombe kadhaa na si kwa shilingi kadhaa". Kwa wanajamii watakaofuata mahari ya binti aliyeolewa hupakwa mafuta ya samli kama ishara ya mibaraka. Mafuta haya hutumika pia wakati wa matambiko kama mafuta ya baraka. Kutokana na umuhimu na thamani ya ng'ombe kwa jamiilugha ya Ginantuzu, baadhi ya wanajamii hulazimika kupewa majina ya ng'ombe na wengine hupewa majina ya mazao ya ng'ombe kama heshima na hadhi kwa wanajamii. Baadhi ya majina yanayotokana na majina ya ng'ombe ni Mang'ombe, Maiku, Nzagamba, Ndilanha, Kadogosa, Idama/Madama, Madale, Bilili, Shuli, Mahala, Gitu Detu, kwa kutaja machache. Majina yanayotokana na mazao ya ng'ombe ni Mabele, Maguta, Mashishanga, Masunga, Masuke, Galiyanda, Mojo, Maboboto, Idili, kwa kutaja machache pia.

**Matokeo ya Utafiti**
Utoaji wa majina ya ng'ombe katika jamii ya Ginantuzu hufuata vigezo mbalimbali. Baadhi ya vigezo hivyo ni rangi ya ngozi, umri au rika, ujinsia, dosari na umbo au maumbile ya ng'ombe. Makala hii ilichunguza majina ya ng'ombe kwa kufuata kigezo cha rangi. Matokeo ya makala hii yamebaini majina kumi na tano (15) ya ng'ombe kwa kwa kigezo cha rangi katika jamii ya

**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1155


Ginantuzu. Jedwali Na. 1 hapa chini linaorodhesha majina ya ng'ombe kumi na tano wanaopatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu kwa kigezo cha rangi.

*Jedwali Na. 1: Majina ya Ng'ombe kwa Kigezo cha Rangi na Ujinsia*

| Na. | Ng'ombe jike | Ng'ombe dume |
|---|---|---|
| 1. | Bilili/balela | Gidalela |
| 2. | Bugondo | Gidabugondo |
| 3. | Buluge | Gituluge |
| 4. | Busheni | Gibusheni |
| 5. | Detu | Gitu |
| 6. | lungu | Gilungu |
| 7. | Holodomu | Gidolodomu |
| 8. | Huumu | Giduumu |
| 9. | Lagini | Gilagini |
| 10. | Mala | Gidamala |
| 11. | Muli | Gidamuli |
| 12. | Samu | Gisamu |
| 13. | Shuli | Gishuli |
| 14. | Sinda | Gisinda |
| 15. | Vashi | Gidavashi |

Ukiangalia kwa makini katika jedwali namba 1, hapo juu utagundua kuwa, majina ya ng'ombe dume yametokana na mashina ya ng'ombe jike. Katika mashina hayo ya ng'ombe jike mofu fulani hupachikwa mwanzoni mwa shina la ng'ombe jike ili kuunda majina ya ng'ombe dume. Mofu hizo hubeba maana ya jinsia ya kiume hata kama maumbo ya mofu yatatofautiana. Wakati mwingine mofu hizo zinazopachikwa kwenye mashina ya ng'ombe jike huweza kuathiri mashina hayo na kutengeneza shina tofauti na la mwanzo lakini maana ikabakia ile ile ya msingi. Mfano mzuri katika jedwali namba 1 hapo juu ni mashina ya namba 1, 3, 5, 7, na 8. Kwa hiyo, matokeo ya utafiti umeonesha kuwa, mofolojia ya shina inatambulisha kwamba ng'ombe anayerejelewa ni jike na uambikaji wa viambishi ***gí-***, ***gid-*** na ***gida-*** hutambulisha kwamba ng'ombe anayerejelewa ni dume.

Ufuatayo ni ufafanuzi wa majina ya ng'ombe kumi na tano (15) kwa jamiilugha ya Ginantuzu:


***1. Bilili/Gidalela:***

**Bilili/balela** ni jina la ng'ombe jike katika jamiilugha ya Ginantuzu ambaye ngozi yake ina rangi nyekundu bila kujali umri. Kiasili neno **bilili** lilitokana na neno **balela**. Kutoka na urahisi wa utamkaji wa neno likageuzwa na kuitwa **bilili**. Gidalela ndilo jina linalopewa ng'ombe dume mwenye rangi kama hii katika jamiilugha ya Ginantuzu. Umbo la ndani la neno ***gidalela*** ni gidaalela. ***Gidaalela*** ni muunganiko wa maumbo mawili yaani *gida* + *alela*. Kwa hiyo, **/a/ + /a/ = irabu moja hudondoshwa.** Kimofolojia, kanuni ya udondoshaji inapotumika katika lugha, sauti moja huachwa au huondolewa na kupelekea kupata neno ***gidalela hapo juu. Gida*** ni mofu inayomaanisha jinsia ya kiume.

Mofu ***gida-*** inapoambikwa kwenye mashina yenye jinsia ya kike, hufanya jina hilo la kike kuwa la kume. Kwa mfano jina *Ng'wasi* katika jamii ya Ginantuzu ni jina la binadamu wa jinsia ya kike ila akiwa wa jinsia ya kiume ataitwa *Gidang'wasi*. Hivyo, neno **bilili/balela** kwa jamii ya Ginantuzu humaanisha ng'ombe jike mwenye rangi ***nyekundu.*** Majina kama *Ilela*/*Malela* (sega/masega ya asali) humaansha rangi hiyo. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 1 hapa chini.

Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1155


*Kielelezo namba 1.*






**BILILI/BALELA** **GIDALELA**

***2. Bugondo/Gidabugondo***

**Bugondo** ni jina la ng'ombe jike katika jamii ya Ginantuzu ambaye ngozi yake ina rangi yenye madoa madogo madogo meupe na nyeusi au meupe na mekundu bila kujali umri. Kiasili neno ***bugondo*** lilitokana na utomvu wa mti mfano wa gundi uliogandamana juu ya magome ya mti husika. Mara nyingi rangi ya utomvu wa mti huwa na rangi nyeupe. Inapotokea ikaganda juu ya mti, mti huo huonekana kuwa na madoadoa meupe huku rangi kuu iliyotawala ni ile ya mti husika. Hivyo basi neno ***bugondo*** katika jamiilugha ya Ginantuzu humaanisha madoa madogo madogo meupe kuwepo kwenye ngozi ya ng'ombe jike mwenye rangi tofauti na nyeupe. Wanajamii wa Ginantuzu wanamwita ng'ombe dume mwenye rangi kama hiyo, ***gidabugondo***. Kimofolojia neno ***gidabugondo*** ni muunganiko wa maumbo mawili ambayo ni ***Gida*** + ***bugondo***. ***Gida*** ni mofu inayomaanisha jinsia ya kiume. Hivyo basi, gidabugondo ni ng'ombe dume mwenye madoa madogo madogo. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 2 hapa chini.

*Kielelezo namba 2*



**BUGONDO** **GIDABUGONDO**

***3. Buluge/Gituluge***

**Buluge** ni jina la ng'ombe jike katika jamii ya Ginantuzu ambaye ngozi yake ina rangi ya waridi. Gituluge ndilo jina analopewa ng'ombe dume mwenye rangi kama hii katika jamii ya Ginantuzu. Umbo la ndani la neno ***gituluge*** ni ***gidbuluge.*** Gidbuluge ni muunganiko wa maumbo mawili ambayo ni mofu tangulizi ***gid-*** inayomaanisha jinsia ya kiume kwa mnyama na shina ***buluge*** lenye maana ya ng'ombe jike. Kimofolojia, fonimu ***d*** + ***b*** huathiriana na kuzalisha fonimu ***t.*** Kitendo cha kuzalisha sauti kama hiyo huitwa **kuimalika kwa fonimu.** Fonimu imeimarika kwa sababu fonimu ***d*** iko chini kiutamkaji imepanda juu na kuwa fonimu ***t.*** Kuimarika kwa fonimu hiyo ndiko kulizalisha neno gituluge yaani ngombe dume mwenye rangi tajwa hapo juu. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 3 hapa chini.

*Kielelezo namba 3.*







**BULUGE** **GITULUGE**

***4. Busheni/Gibusheni***

***Busheni*** ni jina la ng'ombe jike linalopatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Ng'ombe huyu ngozi yake ina rangi nyeusi iliyo na vidoa vidogo vidogo vyeupe. Ng'ombe dume mwenye rangi kama hiyo wanajamiilugha ya Ginantuzu wanamwita ***gibusheni.*** *Neno* ***gibusheni*** limeundwa na muunganiko wa maumbo mawili ambayo ni mofu tangulizi ***gi-*** yenye maana ya jinsia ya kiume na shina ***busheni*** yenye maana ya ng'ombe jike mwenye vidoa vidogo vidogo katika ngozi nyeusi. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 4 hapa chini.

*Kielelezo namba 4.*





**BUSHENI** **GIBUSHENI**

***5. Detu/ Getu***

***Detu*** ni jina la ng'ombe jike anayepatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Ng'ombe huyo hupewa jina hilo kama sifa kutokana na rangi ya ngozi yake kuwa nyeusi tii. Ng'ombe dume mwenye rangi hiyo anaitwa ***gitu*** kwa jamii wa Ginantuzu. Neno ***getu*** umbo lake la ndani ni ***gdetu*** lakini kutokana na michakato ya komofolojia tukapata neno getu. Getu ni muunganiko wa maumbo mawili ambayo ni mofu tangulizi ***g-*** yenye kubeba maana ya jinsia ya kiume na shina ***detu*** lenye maana ya rangi

Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1155


nyeusi kwa ng'ombe jike. Kwa hiyo /g/ + /d/= fonimu /d/ hudodoshwa na kupata getu. hivyo, kanuni ya udondoshaji hupelekea kupata neno getu kama ng'ombe dume mwenye rangi nyeusi.

Kimila, ng'ombe huyu hutumiwa na wataalamu wa mvua kuleta mvua wakati mvua inapoadimika katika maeneo ya wanajamii. Ngozi ya ***gitu*** inatumika kama sanda ya kumfunikia chifu wa Ginantuzu anapofariki. Ng'ombe anayetoa hiyo ngozi huwa hachinjwi bali ananyongwa mpaka kufa kwa kunyimwa pumzi kisha anachunwa. Ng'ombe mweusi katika jamii ya Ginantuzu pia hutumiwa na wazee katika matambiko kama ishara ya kumtukuza Mungu wao. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 5 hapa chini.

*Kielelezo namba 5.*



**DETU**



**GETU**

***6. Lungu/Gilungu***

***Lungu*** ni jina la ng'ombe jike anayepatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Sifa kuu ya ng'ombe huyu ana rangi moja na doa dogo jeupe katikati ya paji la uso wake au kichwani. Ngombe mwenye sifa kama hii anapokuwa dume anaitwa ***gilungu***. Kimofolojia neno gilungu ni muunganiko wa maumbo mawili yaani mofu tangulizi ***gi-*** ikiwa na maana ya *jinsi ya kiume* na shina ***lungu*** lenye maana ya doa dogo jeupe katikati ya paji la kichwa la ng'ombe jike.

Gilungu kama ng'ombe dume katika familia hupewa mamlaka ya uongozi. Kwa kutofautishwa na ng'ombe wengine huvalishwa kengele shingoni kama ishara ya mamlaka. Ng'ombe huyu haruhusiwi kuchukuliwa picha na mtu yeyote isipokuwa kwa ruhusa maalumu. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 6 hapa chini.

**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1155


*Kielelezo namba 6.*






**LUNGU** **GILUNGU**

***7. Holodomu/Gidolodomu***

***Holodomu*** ni jina la ng'ombe jike linalopatikana katika jamii ya Ginantuzu ambaye ngozi yake ina rangi nyeupe iliyo na ueusi kwa mbali kueleke shingoni. Gidolodomu ndilo jina analopewa ng'ombe dume mwenye rangi kama hii katika jamii ya Ginantuzu. Umbo la ndani la neno ***gidolodomu*** ni ***gidholodomu.*** G***idholodomu*** ni muunganiko wa maumbo mawili ambayo ni mofu tangulizi ***gid-*** inayomaanisha jinsia ya kiume na shina h***olodomu*** yenye maana ya rangi nyeupe iliyo na ueusi kwa mbali kueleke shingoni kwa ng'ombe jike. Kimofolojia, fonimu /***d/*** + /***h/*** huathiriana na kufanya tendo la udondoshaji ambapo fonimu /h/ hudondoshwa. Kanuni ya udondoshaji inapotumika katika mazingira kama haya, fonimu /h/ hudondoshwa na kupelekea kupata neon ***gidolodomu.*** Mfano halisi, rejea kielelezo namba 7 hapa chini.

*Kielelezo namba 7.*






**HOLODOMU** **GIDOLODOMU**

***8. Huumu/Giduumu***

***Huumu*** ni jina la ng'ombe jike linalopatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Ngozi ya ng'ombe huyu ina rangi nyekundu iliyochanganyikana na weusi sehemu za shingoni kuelekea kichwani. Giduumu ndilo jina analopewa ng'ombe dume mwenye rangi kama hii katika jamii ya Ginantuzu. Umbo la ndani la neno ***giduumu*** ni ***gidhuumu.*** G***idhuumu*** ni muunganiko wa maumbo mawili


Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1155


ambayo ni mofu tangulizi ***gid-*** inayomaanisha jinsia ya kiume na shina h***uumu*** yenye maana ya ng'ombe jike mwenye rangi nyekundu iliyochanganyikana na weusi sehemu za shingoni kuelekea kichwani. Kimofolojia, fonimu /***d***/ + /***h***/ huathiriana na kufanya tendo la udondoshaji ambapo fonimu /h/ hudondoshwa. Kanuni ya udondoshaji ilipotumika, fonimu /h/ ilidondoshwa na kupelekea kupata neno ***giduumu.*** Mfano halisi, rejea kielelezo namba 8 hapa chini.

*Kielelezo Na. 8 hapa chini.*



***HUUMU***



***GIDUUMU***

**9. *Lagini/Gilagini***

***Lagini*** ni jina la ng'ombe jike linalopatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Ng'ombe huyu ngozi yake ina rangi nyekundu iliyo na vidoa vidogo vidogo vyeupe. ***Gilagini*** ndilo jina analopewa ng'ombe dume mwenye rangi kama hii katika jamii ya Ginantuzu. *Neno* ***gilagini*** limeundwa na muunganiko wa maumbo mawili ambayo ni mofu tangulizi ***gi-*** inayomaanisha jinsia ya kiume na shina ***lagini*** yenye maana ya vidoa vidogo vidogo vyeupe katika ngozi nyekundu ya ng'ombe jike. Mofu ***gi*** imetumika badala ya ***gid*** kwa sababu fonimu ***/d/*** inapokabiliana na fonimu ***/l/*** kanuni ya udondoshaji hujitokeza ambapo fonimu ***/d/*** hudondoshwa na kubaki mofu ***gi***. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 9 hapa chini.

*Kielelezo namba 9.*



**LAGINI**



**GILAGINI**

**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1155


***10. Mala/Gidamala***

***Mala*** ni jina la ng'ombe jike anayepatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Sifa kuu ya ng'ombe huyu huwa na rangi moja na baka kubwa jeupe katika paji lake la uso au kichwani. Ng'ombe huyu hufananishwa na ***lungu*** ila tofauti yake ni ukubwa wa doa jeupe katika paji la uso wake. Ngombe mwenye sifa kama hii anapokuwa dume anaitwa ***gidamala***. Kimofolojia neno ***gidamala*** ni muunganiko wa maumbo mawili yaani mofu tangulizi ***gida-*** ikimaanisha *jinsia ya kiume* na shina ***mala*** lenye maana *doa au baka kubwa jeupa katikati ya paji la uso* au kichwani mwa ng'ombe jike. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 10 hapa chini.

*Kielelezo namba 10.*






**MALA** **GIDAMALA**

***11. Muli/Gidamuli***

**Muli** ni jina la ng'ombe jike linalopatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Ngozi ya ng'ombe huyu ina rangi ya kijivu iliyokolea. ***Gidamuli*** ndilo jina analopewa ng'ombe dume mwenye rangi kama hii katika jamii ya Ginantuzu. *Kimofolojia, neno* ***gidamuli*** limeundwa na muunganiko wa maumbo mawili ambayo ni mofu tangulizi ***gida-*** inayomaanisha jinsia ya kiume na shina ***muli*** yenye maana ya rangi ya kijivu iliyokolea kwa ng'ombe jike. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 11 hapa chini.

Kielelezo namba 11.





**MULI** **GIDAMULI**

***12. Samu/Gisamu***

***Samu*** ni jina la ng'ombe jike linalopatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Ngozi ya ng'ombe huyu ina rangi ya fisi au chui chui. ***Gisamu*** ndilo jina analopewa ng'ombe dume mwenye rangi kama hii katika jamii ya Ginantuzu. *Kimofolojia, neno* ***gisamu*** limeundwa na muunganiko wa maumbo mawili ambayo ni mofu tangulizi ***gi-*** inayomaanisha jinsia ya kiume na shina ***samu*** inayomaanisha rangi ya fisi au chui chui kwa ng'ombe jike. Mofu ***gi*** imetumika badala ya ***gid*** kwa sababu fonimu ***/d/*** inapokabiliana na fonimu ***/s/*** kanuni ya udondoshaji hujitokeza ambapo fonimu ***/d/*** hudondoshwa na kubaki mofu ***gi***. Hivyo, neno ***gisamu*** hutokea. Kimila, Baadhi ya wanajamii huwa ni miiko kwao kumiki aina hii ya ng'ombe. Na wengine hata nyama yao hawawezi kuila wala kuigusa ikihusishwa na mikosi kwa sababu tu ya kufanana na rangi ya fisi. Ng'ombe huyu kimila hawezi kutolewa kama mahari katika suala la ndoa, fidia ama malipo ya aina yoyote. Hata kwenye soko la mifugo katika maeneo husika ana bei ya chini sana akilinganishwa na ng'ombe wengine. Hizo zote ni imani za watu katika eneo husika. Rejea kielelezo namba 12 hapa chini.

*Kielelezo namba 12.*



**SAMU**




**GISAMU**

***13. Shuli/Gishuli***

***Shuli*** ni jina la ng'ombe jike linalopatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Ngozi yake ina rangi nyeupe mwiili mzima bila kujali umri. ***Gishuli*** ndilo jina analopewa ng'ombe dume mwenye rangi kama hii katika jamii ya Ginantuzu. Kimofolojia neno ***gishuli*** limeundwa na maumbo mawili ambayo ni mofu tangulizi ***gi-*** yenye maana ya jinsia ya kiume na shina ***shuli*** ikiwa na maana ya rangi nyeupe kwa ng'ombe jike.

Ng'ombe mweupe katika imani ya Ginantuzu huwakilisa mibaraka kwa familia. Ng'ombe mweupe hupewa heshima yake katika jamii ya Ginantuzu. Jamii hii inapohitaji utakaso wa Mungu katika familia au jamii, ng'ombe mweupe huhitajika kwa ajili ya kutoa kafara kwa Mungu. Kwa baadhi ya familia ng'ombe huyu huvalishi kengele shingoni kwa ajili ya utambulisho. Kwa upande wa soko la mifugo ng'ombe huyu ana bei ghali sana ukilinganisha na ng'ombe wengine sokoni. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 13 hapa chini.

*Kielelezo namba 13.*






**SHULI** **GISHULI**

***14. Sinda/Gisinda***

***Sinda*** ni jina la ng'ombe jike anayepatikana katika jamiilugha ya Ginantuzu. Sifa kuu ya ng'ombe huyu huwa na rangi nyeupe mwishoni mwa mkia wake. Sifa ya ng'ombe huyu mara nyingi huwa na rangi moja isipokuwa mkia wake unakuwa mweupe bila kujali umri. Ng'ombe mwenye sifa kama hii anapokuwa dume anaitwa ***gisinda***. Kimofolojia neno ***gisinda*** ni muunganiko wa maumbo mawili yaani mofu tangulizi ***gi-*** ikimaanisha *jinsia ya kiume* na shina ***sinda*** lenye maana ngombe jike mwenye mkia mweupe. Mazingira ya kutokea kwa mofu ***gi*** rejea kielelezo namba 12 hapo juu. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 14 hapa chini.

*Kielelezo namba 14.*




**SINDA**

***15. Vashi/Gidavashi***

***Vashi*** ni jina la ng'ombe jike linalopatikana katika jamii ya Ginantuzu. Ngozi yake ina rangi ya nyekundu au nyeusi iliyochanganyikana na mabaka makubwa meupe. ***Gidavashi*** ndilo jina analopewa ng'ombe dume mwenye rangi kama hii katika jamii ya Ginantuzu. Kimofolojia, neno ***gidavashi*** limeundwa na maumbo mawili ambayo ni mofu tangulizi ***gida-*** yenye maana ya jinsia ya

kiume na shina ***vashi*** lenye maana ya madoa/mabaka makubwa meupe kwa ng'ombe jike. Mfano halisi, rejea kielelezo namba 15 hapa chini.

*Kielelezo namba 15.*





**Hitimisho**

Makala hii imechambua mofosemantiki na dhima katika majina ya ng'ombe kwa kigezo cha rangi katika jamiilugha ya Ginantuzu. Matokeo ya makala yameonesha kuwa, majina ya ng'ombe dume yameundwa kwa mashina ya ng'ombe jike kwa kuongezewa mofu tangulizi yenye kubeba maana ya jinsia ya kiume, Jumla ya alomofu tatu zenye kumaanisha jinsia ya kiume kwa mnyama zilipatikana. Alomofu hizo ni **gí-, gid-** na **gida-.** Makala pia imeonesha dhima za majina ya ng'ombe baadhi yakihusishwa na dhima za kiimani katika jamii ya Ginantuzu. Mwisho, makala inapendekeza uchunguzi zaidi wa kiisimu juu ya utoaji wa majina ya mifugo kuendelea kufanyika ili kuimarisha mawasiliano katika jamii mbalimbali za wafugaji na kuyahifadhi majina hayo kwa ajili ya vizazi vijavyo.

**Marejeleo**

Batibo, H. M. (1976). *Le Kesukuma: Langue Bantu de Tanzanie: Morphologie & Phonologie.* The de doctorat. Universite de la Sorbonne Nouvelle Paris III.

Brown, G. (1995). *Speakers, Listeners and Communication, Explanation in Discourse Analysis*. Cambridge University Press.

Griffen, E. M. (1997). *A first look at Communication Theory*. Graw Hill Companies Inc.

Imai, I. (1982a). "Subsistence ecology of the pastoral Gabra: A preliminary report." *African Study Monographs, 2*, 1–23.

Imai, I. (1982b). Small Stock Management and the Goat Naming System of the Pastoral Gabra. *African Study Monographs*, Supplementary Issue. 1: 43 - 62.

Mabondo, K. S. (2012), *Negation in Ginantuzu in GinaNtuzu.* Unpublished M.A. (Linguistics). Dissertation, University of Dodoma.

Magoro, A. M., Mtileni, B., Hadebe, K., & Zwane, A. (2022). Assessment of genetic diversity and conservation in South African indigenous goat ecotypes: A review. *Animals, 12*(23), 3353. https://doi.org/10.3390/ani12233353

Masanja, N. (2025). Sababu za Kupungua kwa Matumizi ya Majina ya Asili Nchini Tanzania. Mifano Kutoka Ginantuzu Lahaja ya Kisukuma. *Journal of Kiswahili and Other African Languages,* 3(1), 29-36.
Masija, M.W. (2009). *Investigation of Aspect in Cijita* (Tasnifu ya M.A. Isimu, Haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
Massamba, D. (2004). *Sarufi misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publishers.
Mustefa, A., Abegaz, S., Banerjee, A. G., & Mekasha, Y. (2023). Phenotypic diversity between and within Harar and Ogaden cattle breeds in eastern Ethiopia: The first step for conservation. *Genetic Resources, 4*(7), Article e20230041. https://doi.org/10.46265/genresj.IXPJ9541
Ohta, I. (1987). "Livestock Individual Identification among the Turkana: The Animal Classification and Naming in the Pastoral Livestock Management." *African Study Monographs*, *8(1):* 1 - 69.
Olson, H. (1964). *The Phonology and Morphology of Rịmi*. Hartford Studies in Linguistics.
Peacock, C. (2005). *Goats: Unlocking their potential for Africa's farmers* [Paper presented at the Seventh Conference of Ministers Responsible for Animal Resources, Kigali, Rwanda, October 31–November 4, 2005]
Stephano, R. (2021). "Utoaji Majina ya Mifugo katika Gịrịmi: Uchunguzi wa Gịirwana. *Kioo cha Lugha,* Juz. 19(2). 158-172.
Simon, C. (2024). Critiquing the meaningfulness of Sukuma Cattle names: A non-Philosophical semantic stance. *Journal of Linguistics, Literary and Communication Studies*, *3*(1), 1-9.
Walliman, N. (2011). *Research Methods: The Basic.* Routledge.
Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publishers.